

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**



**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI KUHUSU KUENZISHWA  
KWA MKOA MPYA NA WILAYA MPYA**

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 ina mpa Mamlaka Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania uwezo wa kuigawa nchi kwa kadri ambavyo atakavyoona inafaa.

Aidha, Sheria ya Uanzishaji wa Mikoa na Wilaya Sura ya 397 inamwelekeza Mhe. Rais taratibu za kufuata anapotaka kuanzisha Mkoa na Wilaya.

Kwa kutumia madaraka hayo ya Kikatiba, Rais wa awamu ya nne wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete mnamo tarehe 18/10/2015 alitangaza nia ya kuugawa Mkoa wa Mbeya na kuanzisha Mkoa mpya wa Songwe kwa tangazo la Serikali Na. GN 461.

Aidha, Mhe. Rais katika tarehe hiyo hiyo 18/10/2015 alitoa Tangazo GN. 462 iliyokusudia kuanzisha Wilaya za Songwe, Kibiti, Ubungo, Kigamboni, Malinyi, na Tanganyika.

Tangazo hilo liliweka muda wa wananchi kutoa maoni, ushauri na hata pingamizi, lakini hadi muda wa siku thelathini (30) uliowekwa na Tangazo hilo la Serikali kukamilika hakukuwa na pingamizi lolote lililopokelewa.

Kufuatia hali hiyo, mnamo tarehe 18 Januari, 2016 Rais wa awamu ya tano (5) Mhe. Dr. John P. Magufuli alisaini rasmi Amri ya kuanzishwa kwa Mkoa wa Songwe na Wilaya za;

1. Songwe - (Songwe)
2. Kibiti - (Pwani)
3. Ubungo - (Dar es Salaam)
4. Kigamboni - (Dar es Salaam)
5. Malinyi - (Morogoro)
6. Tanganyika - (Katavi)

Mchakato wa kuanzishwa kwa maeneo haya mapya ya Utawala ulihitimishwa kwa kutolewa Tangazo la Amri ya kuanzishwa kwake katika Gazeti la Serikali kwa GN 69 ya tarehe 29 Januari, 2016 ya kuanzishwa kwa Mkoa wa Songwe, na GN. Na.68 ya kuanzishwa kwa Wilaya za Songwe, Kibiti, Ubungo, Kigamboni, Malinyi na Tanganyika.

Napenda kuchukua fursa hii kuwajulisha wananchi na Umma kwa ujumla kwamba Mkoa wa Songwe umeshanzishwa rasmi kwa mujibu wa Sheria, na vivyo hivyo kwa Wilaya za Songwe, Kibiti, Ubungo, Kigamboni, Malinyi, na Tanganyika nazo zimeanzishwa rasmi kisheria kupitia matangazo tajwa hapo juu.

Nitumie nafasi hii kuwaagiza Wakuu wa Mikoa wote ambao katika Mikoa yao zimeanzishwa Wilaya mpya kufanya maandalizi yote muhimu ili kuwezesha Mikoa na Wilaya hizo kuanza rasmi. Aidha, mkazo uwekwe kwenye upatikanaji wa majengo ya Ofisi na huduma zote muhimu ili kuweka mazingira mazuri ya shughuli za Kiutawala kuanza kufanyika katika maeneo hayo mapya ya Kiutawala.

Imetolewa na,

**Mhe. GEORGE SIMBACHAWENE (Mb)**

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA RAIS -TAMISEMI.**

03 Februari, 2016